JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

SIMU: **0272642152/0715 203188**

SHULE YA SEKONDARI USAGARA,
SLP 330,
TANGA.

Kwa kujibu tafadhali rejea,

Kumb. Na. USS/9/……. **TAREHE: 10.12.2019**

Simu :0715 – 20 31 88/0786 – 20 31 888

JINA LA MWANAFUNZI:……
S.L.P ……..
…….

YAH: <u>MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI USAGARA WILAYA YA TANGA MKOA WA TANGA MWAKA 2020.</u>

1.0 UTANGULIZI:

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga Kidato cha **KWANZA** katika shule hii ya sekondari Usagara mwaka 2020.

Unatakiwa kuripoti shuleni tarehe **06/01/2020** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **17/01/2020** ukiwa umejaza fomu hii kwa usahihi.

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:

i. Sare ya Shule: (***Soma kwa umakini ukurasa namba tatu***)

ii. Picha 3 Passport size kwa matumizi ya ofisi iii. Nakala 1 ya cheti cha kuzaliwa

iv. Daftari/Counter book 10, kalamu, penseli, ufutio, rula, na mkebe wa hesabu

v. Chakula cha wanafunzi wa kutwa, nauli ya kwenda shuleni na kurudi nyumbani pamoja na matibabu. (MZAZI NA MWANAFUNZI)

vi. mzazi hakikisha mwanafunzi anapata matibabu ipasavyo pale anapougua. na

vii. Mahitaji mengine ya kibinadamu kama yapo

2.1 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.

Shule hii ni ya Serikali na inaendeshwa kwa mujibu wa sheria Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, yenye dhamana ya Elimu Nchini na Ofisi ya Raisi – TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na uendeshaji wa Elimu.unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni

(a). Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

(b). Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule nzima.

(c). Kushiriki kwa makini na kufanya maandalio ya jioni (Preparation)

(d). Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine

(e). Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo (f). Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.

(g). Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa

(h). Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na

(i). Kutunza mali za Umma

2.2 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha ukafukuzwa shule:

i. Wizi ii. Uasherati na ushoga iii. Ubakaji

iv. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli n.k.

v. Kupigana au kupiga vi. Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma

vii. Kudharau Bendera ya Taifa viii. Kuoa na kuolewa ix. Kuwa mjauzito/kupata mimba x. Kutoa mimba

xi. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga Amani na usalama wa shule au watu

xii. Kukataa adhabu kwa makusudi

xiii. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi

2.3 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa shuleni na mwanafunzi

(a). Medical Examination Form nayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospital ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.

(b). Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

(c). Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule

2.4 Tafadhali soma kwa makini maelekezo / maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

……

MKUU WA SHULE

MAELEKEZO YA ZIADA KUHUSU SARE YA SHULE YA SEKONDARI USAGARA.

WASICHANA:

i. Shati mbili (2) za mikono mifupi zisizo na urembo wowote na zisizobana (slimfit) zenye vifungo mbele. ii. Sketi (2) zilizochanua zenye rinda box mbele na nyuma na marinda madogomadogo pembeni za rangi ya ugoro, zinazofunika magoti na zisizo onesha (not transparent) mwili kwa ndani.

iii. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba na visivyokua na visigino virefu. iv. Soksi nyeupe pair mbili (2).

v. Kuweka baa moja kwenye shati katika bega la mkono wa kushoto ikimaanisha kidato cha kwanza (I) tumia kitambaa cha rangi ya ugoro.

vi. Ikiwa atahitaji kuvaa sweta, avae sweta la rangi ya ugoro (brown) la mikono mirefu, shingo ya V nalisiwe na maua. vii. Kwa waislamu wanaopenda kuvaa **HIJABU**, wanaruhusiwa kuvaa Hijabu ifuatayo:-

(a). Shati nyeupe ya mikono mirefu (pea mbili) iliyoshonwa kwa kutumia kitambaa cha Tetron/Cotton.

(b). Sketi (2) zilizochanua ndefu hadi kwenye kifundo cha mguu zenye rinda box mbele na nyuma na marinda madogomadogo pembeni za rangi ya ugoro, zisizobana na zisizopitisha mwanga (not transparent) kuonesha mwili wa ndani.

(c). Kitambaa cheupe cha kichwani **(juba)** cha duara kinachoishia kwenye mwisho wa mikono iwe tetroni/Cotton

(d). Kuweka baa moja kwenye juba upande wa kushoto chini ikimaanisha Kidato cha kwanza (I) tumia kitambaa cha rangi ya ugoro.

WAVULANA:

i. Mashati mawili meupe ya mikono mifupi na yasiyobana
ii. Suruali mbili za rangi ya ugoro zenye marinda mawili zisizobana inchi 16 upana
iii. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba, visivyokuwa na visigino virefu na vile vile visiwe aina ya “boots”
iv. Soksi nyeupe pea 2
v. Ikiwa itahitajika kuvaa sweta, avae sweta la rangi ya ugoro, (brown) la mikono mirefu, shingo ya V na lisiwe na maua.
vi. Mkanda mweusi usio na marembo
vii. Kuweka baa moja kwenye shati katika bega la mkono wa kushoto ikimaanisha kidato cha kwanza (I)

Mzazi/Mlezi zingatia maelezo ambayo yametolewa, Mzazi/Mlezi ambaye atashona sare ya shule kinyume na maelezo, basi sare hiyo haitakubaliwa na uongozi wa shule.

NB: Mwanao ajapo shule kabla ya kushonewa sare ya Usagara, aje na sare yake ya shule ya msingi asije na nguo za nyumbani.

SARE ZA MICHEZO:

WAVULANA/WASHICHNA : Fulana rangi nyekundu au bluu zisizo na maandishi na Bukta za rangi nyekundu au bluu

VIATU: Raba za michezo rangi yoyote

PICHA YA MWANAFUNZI

FOMU YA KUKUBALI KUJUNGA

MWANFUNZI:

Mimi…….nakubali kuchukua nafasi niliyopewa Kidato cha **KWANZA** katika shule ya Sekondari USAGARA. Ninaahidi kufuata sheria na masharti yote ya shule.

Saini ya Mwanafunzi……Tarehe: ……

HATI YA MZAZI KUKUBALI MASHARTI YA SHULE

Mimi……
Mzazi/Mlezi wa……nimesoma na kuyakubali masharti yote ya mwanangu kujiunga na shule ya sekondari Usagara. Pia nitasimamia utekelezaji wa sheria za shule alizopewa. Najua pia kuwa simu, utoro na uchelewaji shuleni **HAVIKUBALIKI.**

PICHA YA MZAZI/MLEZI

Saini ya Mzazi/Mlezi…….

Anwani ya Mzazi/Mlezi……

……..

Namba ya simu ya Mzazi/Mlezi……...

DOLE GUMBA →

JINA LA KATA: _____

JINA LA MTENDAJI KATA: _____

NAMBA YA SIMU: _____

SAINI: _____ **MHURI** →

USAGARA SEC. SCHOOL
P.O.BOX. 330,
TANGA.

MEDICAL EXAMINATION FORM

PART A

To Medical Officer,
.....
.....
.....

MR/MISS.....(Name in full)
Please examine the above named student as to his/her physical and mental fitness for a full time schooling course.The examinations should include the following categories (III) each category or sub-category of which will render the applicant in-eligible in case of a defect. Pregnarcy (category IV) will also render a girl candidate inligible for the course.

I (a) Eye-sight (b) Hearing
(c) Limbs
(d) Speech
(e) Venereal Diseases(s)
(f) Leprosy
(g) Epilepsy

II. Neurosis

III. Other serious disease

Signature……

PART B

MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by Government Medical Officer)
I have examined the above named and consider that he/she is physically fit/unfit and mentally fit/unfit for a full time school course.

I (a) Eye-Sigh…….
(b) Hearing……
(c) Limbs……..
(d) Speech……...
(e) Venereal Diseases……..
(f) Leprosy……...
(g) Epilepsy…….

II. Neurosis
III. Other serious disease
Station……
Signature……

Designation…… Date……